**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI JUU YA UKIUKWAJI WA HAKI ZA WAFUGAJI NA AMRI ZA MAHAKAMA KUHUSU KESI ZA WAFUGAJI NCHINI TANZANIA**

## A. Utangulizi

Taarifa hii kwa vyombo vya Habari inakuja kufuatia ukiukwaji wa haki za binadamu, utawala Sheria, ukiukwaji wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kupuuzwa au kudhauriwa kwa maamuzi na amri za Mahakama unaofanywa na baadhi ya viongozi na watumishi wa Serikali.

Ni muhimu kukumbuka kwamba, mnamo tarehe 10.06.2022 Serikali kwa kutumia nguvu na bila kufuata Sheria ilianza kuweka vigingi katika eneo la vijiji 14 vilivyopo katika tarafa ya Loliondo na sehemu ya tarafa ya Sale wilayani Ngorongoro. Matumizi ya nguvu ya vyombo vya dola yalipelekea wananchi kadhaa kupigwa risasi, kupotezwa, kujeruhuiwa na kuondolewa katika ardhi yao bila ridhaa yao. Maelfu ya wananchi walikimbilia nchi jirani ya Kenya kwa ajili ya usalama wa maisha yao na wengine kutafuta makazi ya muda kwa ndugu zao kokote kule kwaajili ya kujihifadhi. Kabla ya utwaaji wa ardhi hiyo yenye ukubwa wa kilometa za mraba 1,502 ardhi yenye jumla ya vijiji 14, takribani viongozi wote wawakilishi wa maeneo hayo walikamatwa na kuwekwa kizuizini kwa takribani miezi sita ambapo waliachiwa baada ya kukamilika kwa utwaaji wa ardhi katika maeneo wanayowakilisha.

Mnamo tarehe 17.06.2022, Waziri wa Mali Asili na Utalii alitangaza kuwa ardhi hiyo inayojumuisha vijiji 14 ambayo ina ukubwa wa kilometa za mraba 1,502 kuwa Pori Tengefu la Pololeti kupitia Tangazo la Serikali Na. 421 la 2022. Tangazo la Waziri lilipingwa na wananchi wa maeneo yaliyoathirika kupitia Shauri No. 21 la Mwaka 2022. Wakati shauri dhidi ya tanagazo la Waziri wa Maliasili na Utalii likiendelea Mahakamani, mnamo tarehe

14.10.2022, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alitangaza eneo hilo hilo kuwa Pori la Akiba la Pololeti kupitia  Tangazo la Serikali Na. 604 la Mwaka 2022. Vilevile Tangazo la Rais lilipingwa kwenye Mahakama Kuu ya Tanzania kanda ya Arusha na wananchi walioathirika na tangazo hilo kupitia shauri Na. 178 la Mwaka 2022 ambapo wananchi hao waliomba ridhaa ya Mahakama ili kuwasilisha maombi ya mapitio ya Tangazo hilo la Rais (yaani *Judicial Review*) kama lilizingatia Sheria.

Mnamo tarehe 22.08.2023 Mahakama Kuu ya Tanzania kanda ya Arusha ilitoa ridhaa kwa wananchi kuwasilisha maombi ya mapitio ya Tangazo hilo la Rais. Muhimu zaidi, wakati Mahakama Kuu inatoa ridhaa ya kufungua kesi ya msingi kwa wananchi hao walioathirika, ilitoa amri pia ya kusimamishwa utekelezaji wa Tangazo la Serikali Na.604 la Mwaka 2022 ambalo lilitangaza eneo lenye mgogoro kuwa Pori la Akiba la Pololeti hadi kesi ya msingi itakapoisha. Kesi ya msingi iliyofunguliwa baada ya maamuzi hayo ya Mahakama Kuu ilifunguliwa mara moja na kupewa namba 18 ya Mwaka 2023, kesi hii ya msingi ipo katika hatua za kusikilizwa.

Vilevile, mnamo tarehe 19.09.2022, Mahakama Kuu ya Tanzania kanda ya Arusha ilitoa uamuzi juu ya Tangazo la Waziri wa Mali Asili na Utalii Na. 421 la Mwaka 2022 ambapo pamoja na mambo mengine Mahakama ilitamka kuwa Tangazo la Waziri halikufuata utaratibu wa Kisheria hasa kuwashirikisha wananchi wakazi wa vijiji hivyo, kata, Halmashauri ya Wilaya pamoja na wahanga wa Tangazo hilo.

***Katika uamuzi huo, Mahakama ilisisitiza kwamba:***

a) Pori Tengefu la Pololeti lenye kilometa za mraba 1,502 halikutangazwa kwa kufuata Sheria na lilikufa mara baada ya Rais kutangaza kuwa eneo hilo ni Pori la Akiba kupitia Tangazo la Serikali Na. 604 la mwaka 2022 na hivyo kwa sasa hakuna kitu chochote kiitwacho Pori Tengefu la Pololeti
b) Utekelezaji wa Tangazo lililotolewa na Rais Na. 604 la Mwaka 2022 usimame kuanzia tarehe 22.08.2023 hadi kesi ya msingi itakapoisha kwa kutolewa uamuzi na Mahakama.

**B. Kutokuheshimiwa kwa Amri za Mahakama**

Baada ya Mahakama kutoa amri ya kusimamisha utekelezaji wa Tangazo la Rais Na.604 la Mwaka 2022 na pia kusema kuwa Tangazo la Waziri lilikoma baada ya tangazo la Rais kutolewa, maafisa wa Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro na vyombo vya ulinzi na usalama waliendelea kukamata mifugo ya wananchi iliyoonekana kuwa karibu au ndani yae neo la

Pololeti, kuwakamata na kuwapiga wananchi, kukamata mifugo ya wananchi, kutoza faini ya shilingi laki moja kwa ng'ombe mmoja na shilingi elfu ishirini na tano kwa kila mbuzi au kondoo na wengine mifugo yao imepigwa risasi au kutaifishwa moja kwa moja.

Yote haya yanafanyika kwenye eneo ambalo kuna amri ya zuio la Mahakama. Mfano mnamo tarehe 31.10.2023, Serikali ilipeleka kesi katika Mahakama ya wilaya ya Ngorongoro (Kesi Na 01 ya Mwaka 2023) iliyopo Loliondo ili kutaifisha mifugo iliyokamatwa katika eneo ambalo kuna zuio la Mahakama Kuu. Mkurugenzi wa Mashtaka Nchini (DPP) hata hivyo aliondoa maombi yake baada ya kugundua kuwa hakuna Sheria ya kushikilia mifugo hiyo. Ijapokuwa Serikali iliondoa kesi hiyo Mahakamani lakini maafisa wa wanyamapori wamekataa kuachia mifugo hiyo hadi ilipwe faini ya laki moja kwa kila ng'ombe.

Watumishi wa Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro wamekuwa wakikamata mifugo, kuinyima maji, malisho ili mifugo hiyo iwe dhaifu ili wamiliki walipe faini kwa kuogopa mifugo yao kuwa itakufa kwa njaa.

Mnamo tarehe 04.10.2022, wakili wa Serikali katika taarifa yake kwa umma juu ya uamuzi wa Mahakama alishauri kuchukuliwa kwa hatua ambazo zitapelekea oparesheni kufanyika kwenye eneo ambalo kuna zuio la Mahakama.  Wananchi wa Loliondo wamekuwa wakipigwa na askari wa Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro na vyombo vingine vya ulinzi na usalama ili kuwatisha waondoke kwenye eneo la vijiji lenye kilometa za mraba 1,502 kama njia ya kuwatisha watu kuachia ardhi yao halali.

Mbali na matukio hayo mnamo tarehe 31/10/2023, Mamlaka ya Hifadhi za Taifa (TANAPA) ilifungua kesi katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Musoma kuomba kupewa amri ya kuuza mifugo zaidi ya 1,000 kama mali isiyokuwa na mmiliki wakati kiuhalisia mifugo hiyo ni mali ya wakazi wa Loliondo. Wakati utaratibu huu unafanyika, TANAPA walikuwa wakijua fika ni nani ndio mmiliki wa Mifugo hiyo, siku moja baadae yaani tarehe 01.11.2023 Mahakama Kuu ya Tanzania kanda ya Musoma ilitoa amri ya kusimamisha uuzwaji wa mifugo hiyo 1,000 iliyokuwa hatarini kuuzwa na TANAPA.

Hata hivyo, zuio hilo la Mahakama Kuu halikuheshimiwa na mifugo yote iliuzwa pamoja na kufahamu uwepo wa amri ya Mahakama Kuu. Wamiliki wa mifugo hiyo wametueleza kwamba namna amri ya kuuza mifugo hiyo ilivyopatikana katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Musoma iliwapa mashaka kwasababu shauri hilo liliendeshwa siku moja na siku hiyohiyo amri ya kuuza mifugo ilitolewa bila wito au notisi kutolewa kwa wamiliki wa mifugo hiyo kujitokeza mahakamani kwaajili ya kutoa utetezi wao. Tangazo la kuuzwa mifugo hiyo lilitolewa siku hiyohiyo na kuuzwa wakati amri ya kusimamishwa kuuzwa kwa mifugo hiyo ilitolewa na

Mahakama Kuu. Wamiliki wa mifugo wanaeleza kuwa mifugo yao iliingizwa hifadhini na maaskari wa Ngorongoro kwa kushirikiana na wengine kutoka hifadhi ya Taifa ya Serengeti.

Unyanyasaji huu hautokei katika wilaya ya Ngorongoro pekee, bali na maeneo mengine nchini. Kwa mfano, katika wilaya ya Mbarali, TANAPA walikamata mifugo na kuwaingiza katika hifadhi ya Taifa ya Ruaha. Kijana mmoja aliyejaribu kuwazuia mifugo hao kuingizwa hifadhini ili maaskari wasije kudai kwamba mifugo hiyo ilikuwa hifadhini, kijana huyo anadaiwa kuuwawa kwa kushambuliwa na maaskari wa TANAPA. Baadae Mifugo hiyo iliuzwa kama mali isiyo na mwenyewe japokuwa inajulikana kuwa familia ya aliyeuwawa ndio wamiliki wa mifugo hiyo. Baadae, Baba Mzazi wa kijana aliyeuwawa alikamatwa kama sehemu ya kumtisha pamoja na kuwa alitokea safarini Sumbawanga na hakuwepo wakati tukio hilo linatokea. Kukamatwa kwa mmiliki wa mifugo ambaye ni Baba wa kijana aliyeuwawa inaeleza bayana kuwa wamiliki wa mifugo walijulikana japo mifugo yao imeuzwa kama mifugo isiyo na mwenyewe.

Vilevile katika Wilaya ya Tarime mkoani Mara, wafugaji wamekuwa wakinyanyaswa pamoja na wananchi kunyang'anywa maeneo yao kinyume cha Sheria hali hii ilipelekea wenyeviti wa vijiji 14 kujiuzulu kutokana na unyanyasaji huo wa wananchi.

Vitendo hivi sio tu vinakiuka haki za mifugo, haki za binadamu na Katiba ya nchi yetu, lakini pia ni shambulio kwa uhuru wa Mahakama na utawala wa Sheria nchini kwetu. Vitendo hivi pia vinapelekea wananchi wa kawaida kuamini kwenda Mahakamani ni kupoteza muda, kuhatarisha amani na ni dalili za uwezekano wa wananchi kuchukua Sheria mkononi jambo ambalo litaleta uvunjivu wa amani.

**C. Wito Wetu**

i. Tunalaani vikali ukiukwaji wa haki za mifugo katika wilaya ya Ngorongoro na maeneo mengine kote nchini ambapo mifugo imekuwa ikikamatwa kinyume cha Sheria, kuuzwa ama kutaifishwa Kinyume cha Sheria na Katiba ya nchi yetu.

ii. Tunalaani vikali vitendo vyote ambavyo vimeonekana kupuuza ama kudharau maamuzi na amri halali za Mahakam ana kupelekea mifugo kuuzwa kinyume cha Sheria za nchi yetu.

iii. Tunatoa wito wa kuchukuliwa hatua za kisheria kwa watumishi wa Mahakama ambao wanashiriki kuhujumu na kuwafilisi wafugaji kwa kutoa amri ya kutaifisha na kuuza mali zao bila taratibu za kisheria za kutoa wito kwa wahusika kwenda mahakamani.

iv. Tunatoa wito kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuwaelekeza watumishi wa Serikali hasa katika maeneo lalamikiwa kuheshimu maamuzi na amri za Mahakama kwani amri za Mahakama zinapaswa kuheshimiwa na kila mtu.

v. Tunatoa wito kwa TANAPA na Jeshi la Polisi kuacha mara moja ukamataji wa mifugo kwenye maeneo ambayo kuna zuio la Mahakama na waache kuwasumbua wafugaji kwani nao wana haki ya kumiliki mifugo kama mali halali kwa mujibu wa ibara ya 24 ya Katiba ya nchi yetu.

vi. Tunalaani kitendo cha watumishi wa Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro kutesa mifugo kwa kuwanyima malisho na maji ili kufanya wamiliki kulipa faini kwa kuhofia mifugo yao kufa.

vii. Tunatoa wito kwa watumishi wa hifadhi za Taifa waache tabia ya kuswaga mifugo ya watu na kuingiza hifadhini kwa lengo la kutoza faini, kutaifisha na kuuzwa kwa mifugo hiyo.

viii. Tunatoa wito kwa Serikali kuwachukulia hatua za kisheria watumishi na viongozi wa Serikali walioshiriki katika ukiukwaji wa amri za Mahakama. Lengo ni kuhakikisha kwamba watumishi hao wanaheshimu na kulinda utawala wa Sheria na katiba ambayo waliapa kuilinda.

ix. Tunatoa wito kwa Jeshi la Polisi kufanya uchunguzi wa mauaji yaliyotokea Mbarali, kutoa taarifa kwa umma na kuchukuliwa hatua kwa wahusika kwa mujibu wa Sheria.

x. Pia tunatoa wito kuhusu mifugo yote iliyouzwa bila kufuata utaratibu wa kisheria, wahusika wote waliouza walipe wenyewe ili iwe funzo kwa wengine wanaokiuka Sheria za nchi yetu.

xi. Tunatoa wito pia kwa Mahakama ya Tanzania kufuatilia utekelezaji wa maamuzi yake kwa wivu mkubwa, sisi tunaamini kwamba maamuzi ya Mahakama ni maamuzi ya haki na hivyo yanapaswa kutekelezwa na kila mtu kama yalivyoamuliwa.

xii. Tunatoa wito wa jumla kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kutekeleza maamuzi mbalimbali ya Mahakama kisheria. Mfano maamuzi ya Mahakama za ndani, za Kikanda na Kimataifa. Maamuzi hayo ni kama ya kesi ya Rebecca Gyumi, Maria Mushi, Mjomba Mjomba, Kesi ya THRDC, LHRC na MCT iliyoamuliwa na Mahakama ya Haki ya Afrika Mashariki Mwaka 2019, THRDC na LHRC iliyoamuliwa na Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu, kesi za Mch. Mtikila, kesi ya Jebra Kambole na kesi ya Bob Wangwe ya Wakurugenzi wa Uchaguzi

zilizoamuliwa na Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu na zingine nyingi.

Imetolewa na Mashirika yafuatayo:

1. **Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC)**
2. **Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC)**
3. **Baraza la Wanawake Wafugaji (PWC),**
4. **Shirika la Uraia na Msaada wa Kisheria (CILAO)**
5. **Mtandao wa Mashirika ya Kifugaji (PINGOs Forum)**
6. **Ujamaa Community Resource Team (UCRT)**
7. **Shirika la Kukuza Haki za Binadamu (OPH)**
8. **Jukwaa la Katiba Tanzania (JUKATA)**
9. **Chama Cha Wafugaji Tanzania (CCWT)**
10. **Shirika la Uhifadhi wa Mifumo ya Asili na Jadi (TEST)**
11. **Shirika la Maendeleo Jumuishi Wilayani Ngorongoro (IDINGO)**
12. **Jukwaa la Ardhi Tanzania.**
13. **Shirika la Kuinua na Kusaidia Maisha ya Wafugaji (PALISEP)**
14. **Jumuiko la Maliasili Tanzania (TNRF)**
15. **Green Planet Initiative (GPI)**
16. **Pan African Lawyers Union (PALU)**

**November 08, 2023**

**Dar es Salaam, Tanzania**